

**TAARIFA YA UNUNUZI WA UFUTA KWA NJIA YA MINADA MSIMU 2017/2018
MKOA WA LINDI.**

UTANGULIZI

Mkoa wa Lindi umeanza kutekeleza mfumo mpya wa mauzo ya zao la ufuta mwaka 2017/2018, ambapo mfumo unaotumika ni mfumo wa ukusanyaji wa zao la ufuta kwenye ghala za vyama vya Ushirika vya msingi na kuuzwa kwa njia ya minada. Mfumo huu ni sawa na mfumo wa stakabadhi ghalani isipokuwa katika mfumo huu hakuna ghala zilizosajiliwa na kupewa leseni kama ilivyo katika mfumo wa stakabadhi ghalani.

Msimu wa ukusanyaji na uuzwaji wa zao la ufuta mwaka huu (2017/2018) kimkoa ulifunguliwa rasmi tarehe **01/06/2018** ambapo mnada wa kwanza ulifanyika tarehe **18/06/2018** katika maeneo ya chama cha msingi cha **Pachani** kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Lindi. Hadi kufikia sasa imefanyika **minada 15** iliyokuwa ikisimamiwa na vyama vikuu vya Lindi Mwambao na RUNALI.

Aidha katika msimu huu, mkoa ulilenga kukusanya na kuuza zaidi ya **tani 38,273,000** za ufuta kutoka katika maeneo ya halmashauri za wilaya na Manispaa ambapo jumla ya vyama vya msingi vya **ushirika 130** vinashiriki.

UFANYIKAJI WA MINADA

Minada ya uuzwaji wa zao la ufuta inaratibiwa na kufanywa na vyama vikuu vya Ushirika vilivyopo katika mkoa wetu. Chama kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao kinaratibu na kufanya minada ya mauzo ya ufuta katika Halmashauri za Wilaya za Lindi, Kilwa na Manispaa ya Lindi na Chama kikuu cha Ushirika cha RUNALI kinaratibu na kufanya minada ya mauzo ya zao la ufuta katika Halmashauri za Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale.

Aidha, minada ya mauzo ya ufuta imekuwa ikifanyika kila **Jumapili na Jumatatu** ambapo chama kikuu cha Ushirika cha **Lindi Mwambao** hufanya mnada kila Jumapili na Chama kikuu cha Ushirika cha **RUNALI** hufanya mnada kila Jumatatu.

MAUZO YA UFUTA

Mkoa umefanya jumla ya minada kumi na **tano (15)** ambapo hadi kufikia **tarehe 06/08/2018** jumla ya **kilo 30,307,068** za ufuta zenye thamani ya **shilingi 88,566,623,312** zimeuzwa. Chama kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao kimefanya minada nane (8) wakati chama kikuu cha Ushirika cha RUNALI kimefanya minada saba (7). Mchanganuo wa mauzo haya kihalmashauri ni kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa mauzo ya ufuta kihalmashauri

NA.	HALMASHAURI	MAKISIO 017/2018 (KGS)	KIASI KILICHOKUSANYWA NA KILICHOUZWA (KGS)	THAMANI YA MAUZO (TSHS)
1	KILWA	15,000,000.00	11,251,759.00	32,541,496,582.00
2	HALMASHAURI YA LINDI	5,065,000.00	3,197,695.00	9,373,122,574.00
3	LINDI MANISPAA	750,000.00	470,674.00	1,362,454,891.00
4	NACHINGWEA	4,500,000.00	4,070,862.00	12,138,915,018.00

5	LIWALE	4,958,000.00	5,498,988.00	16,001,401,891.00
6	RUANGWA	8,000,000.00	5,817,090.00	17,149,232,356.00
	JUMLA	38,273,000.00	30,307,068.00	88,566,623,312.00

Chanzo; Halmashauri

MCHANGANUO WA MINADA KWA KILA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA

Jedwali Na. 2: Idadi ya minada kwa kila chama kikuu cha ushirika

Na.	Chama kikuu	Mkisio 2017/2018	Idadi minada	Mauzo (kilo)	Asilimia	Thamani
1	Lindi Mwambao	20,815,000	8	14,920,128	71.68%	43,277,074,047
2	RUNALI	17,458,000	7	15,386,940	88.14%	45,289,549,265
	JUMLA	38,273,000	15	30,307,068	79.19%	88,566,623,312

MCHANGANUO WA UKUSANYAJI NA UUZWAJI WA UFUTA KWA KILA MNADA KATIKA KILA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA.

JedwaliNa. 3: Mchanganuo wa mauzo ya ufuta kwa kila mnada kuanzia tarehe 01 Juni 2018 hadi tarehe 06/08/2018.

MNADA	CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA-LINDI MWAMBAO UNION (KGS)	THAMANI (TSHS)	CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA-RUNALI (KGS)	THAMANI (TSHS)
1	835,646	2,264,600,660	607,115	1,720,806,138
2	2,267,785	6,368,690,671	1,827,940	5,369,993,125
3	2,961,052	8,576,226,011	3,101,576	9,435,953,330
4	2,738,132	8,214,631,921	3,471,539	10,460,811,825
5	2,501,033	7,486,201,493	3,753,713	10,779,054,327
6	786,549	2,361,847,041	1,952,085	5,399,457,140
7	2,076,478	5,783,226,859	762,468	2,123,473,380
8	792,597	2,221,649,391		
JUMLA	14,920,128	43,277,074,047	15,386,940	45,289,549,265
MAKISIO	20,815,000		17,458,000	
ASILIMIA	71.68%		88.14%	
MAKISIO KIMKOA		Kilo 38,273,000		
MAKUSANYO SASA		Kilo 30,307,068		
ASILIMIA KIMKOA		79.19%		

NB:

Zipo tozo mbalimbali ambazo anakatwa mkulima na mnunuzi wa zao la ufuta kama ifuatavyo:-

Mkulima anakatwa tozo zifuatazo

- Chama Kikuu Sh. 10
- Chama cha Msingi cha Ushirika Sh. 60
- Usimamizi Mkoa Sh. 2
- Usimamizi Halmashauri Sh. 1
- Mfuko wa Maendeleo ya Elimu Sh. 30

Hivyo kwa ujumla mkulima anakatwa Sh. 103 tu kwa kilo.

Kwa upande wa Mnunuzi anakatwa tozo zifuatazo,

- 3% ya soko ya mnada
- Chama Kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao Sh. 15
- Chama Kikuu cha Ushirika cha RUNALI Sh. 16

Imetolewa na:

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,

S.L.P. 1054,

LINDI.

18/08/2018